

# EE BABA MIKONONI MWAKO


Wimbo wa katikati "IJUMAA KUU"

**Na John D. Kajala**
**20.3.2004 - Tanga**

**Zab. 31:1, 5, 11 - 13a, 14 - 16, 24**



1. Nimekukimbilia wewe Bwana, nisiaibike Milele / Kwa haki yako uniponye, mikononi mwako naiweka roho yangu, umenikomboa Ee Bwana Mungu wa kweli.

2. Kwa sababu ya watesi wangu nimekuwa laumu, Naam, hasa kwa jirani zangu / Na kitu cha kutisha kwa rafiki zangu, walioniona njiani walinikimbia.

3. Nimesahauliwa kama mfu asiyekumbukwa, nimekuwa kama chombo kilichovunjika / Maana nimesikia masingizio ya wengi, hofu ziko pande zote.

4. Lakini mimi nakutumaini wewe Bwana, nimesema, wewe ndiwe Mungu wangu / Nyakati zangu zimo mikononi mwako, uniponye na adui zangu, nao wanaonifuatia.

5. Umwangaze mtumishi wako, kwa nuru ya uso wako, uniokoe kwa ajili ya fadhili zako / Iweni hodari, mpige moyo konde, ninyi nyote mnaomngoja Bwana.